TANGAZO LA SERIKALI NA. 469 la tarehe 14/7/2023

SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI,

(SURA YA 20)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 204(1))*

AMRI YA UTEUZI WA MTAALAM WA ALAMA ZA VIDOLE YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uteuzi wa Mtaalam wa Alama za Vidole ya mwaka, 2023.

Uteuzi wa mtaalam wa alama za vidole

2. Mtu ambaye jina lake limetajwa kwenye Jedwali la Amri hii ameteuliwa kuwa Mtaalam wa Alama za Vidole kwa madhumuni ya kutoa ripoti kama ushahidi katika mashauri ya jinai au katika mambo yanayohusiana.

Uhalali wa uteuzi

3.-(1) Uteuzi uliofanywa chini ya Amri hii utakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Amri hii.

(2) Bila ya kujali ujumla wa aya ndogo ya (1), mtu aliyeteuliwa kama mtaalam wa alama za vidole chini ya Amri hii anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kinachopungua miaka mitano pale ambapo ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma itakoma au uteuzi wake utasitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

*Tangazo La Serikali Na. 469 (Linaendelea)*

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| S/N | NAMES |
|---|---|
| 1. | Violeth Onesmo Kiluvia |

Dodoma
21 Juni, 2023

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU,
*Mkurugenzi wa Mashtaka*